**Mzee Leshonde:** Wasitolewa kwa masomo, ili wauuzwe, waolewe, kwa maana hii inaendelea. Na sijui kwa nini watu hawajajua kwa maana kwa upande yetu Wamaasai ile biashara ya wasichana hakuna tena. Unakuta wengi wanakaa kwa mabona, wana zaa; kwa hivyo kunyang'a msichana haki yake ni mbaya.

Kwa hivyo sina mingi.

**Com. Lethome:** Mzee Ole Musa, tunakupatia nafasi hii na useme jambo la .....(inaudible) na kuna waalimu wawili. Umfuat..... (inaudible) Haya endelea.

**Kerenko Ole Musa:** *kaji taa sinanu kirrinkol ole Musa*

**Translator:** Naitwa Mwana Kerenko Ole Musa.

**Ole Musa:** *ore nai nanu anaa enayieu naa kore enkisuma neaku enepesho*

**Translator:** Amesitisiza sana masomo ya shule ya msingi na watoto wasome bila kulipa karo.

**Ole Musa:** *amu kumok iltung`ana lemeidim atalak*

**Translator:** Kwa sababu kuna watu wengi wasiojiweza upande wa Maralal.

**Ole Musa:** *naa pooki ake pee edupayu olosho enkop kwa ujumla teneisumate iltung`ana*

**Translator:** Naonelea ili watu Fulani, kama Wamaasai waweze kupata nguvu bila watu waliosoma hawatajiweza.

**Ole Musa:** *eyieu naaji naa ore naaji kila oltun`gani nening ena kutuk e taifa nairorita pooki ng`ae*

**Translator:** Napendelea kwamba kama masomo haya yangetolewa kwa sababu watu wangeweza kujua lugha hizi za kitaifa ambazo zinazungumzwa.

**Ole Musa:** *naa teneitauni enkisuma e pesho neidimi ataraki enkera sukul*

**Translator:** Na njia ambaye hiyo itawezekana ni kutoa shule bure, masomo yawe ni bure, shule msingi.

**Interjection:** Something else. Sasa unajua anarudia hivi, amesha pendekeza masomo ya bure ama ni ..... (inaudible)

**Translator:** Vikundi ambazo ni za miradhi ziangaliwe.

**Ole Musa:** *ore eniare naa kajo peyie eing`ori projeki iturrurri nayieu neing`orr serkali amu ore taata ninche yiook*

*kiata scheme kiata inkang`itie nageluno naketumo iltung`ana okuni nenyi ropiyiani oo ltung`ana nemeta entoki nasuj*

**Translator:** Serikali isimamie sisi kwa sababu ametoa mfano hizi tunaita Cultural Bomas. Watu wawili watatu wanachaguliwa, chochote kinachopatikana pale, wanakisambaza bila kurudisha wenzao

**Ole Musa:** *ore tene wei oo nkulukuo nayieu najo ore embusel ewaki tenkoitoi torrono*

**Translator:** Kwa upande wa ardhi, kwa mfano Amboseli ilinyakuliwa kwa njia mbaya.

**Ole Musa:** *ore magadi ewaki te nkooitoi torrono*

**Translator:** Upande wa Magadi vile vile ilichukuliwa kwa njia mbaya.

**Ole Musa:** *nikiyieu nishukokini yiook*

**Translator:** Tunaomba sana ile ardhi irudishiwe wenyewe.

**Ole Musa:** ore tene wei e county council ayeiu naji nanu enata enata meidim olkasolai aishooi implotini openy

**Translator:** Kurudi upande wa serikali ya mitaa, nguvu zinazowaruhusi Madiwani kupeana ardhi ziondolewe.

**Ole Musa:** *nayieu naaji ore peyie eponu eweji naijo Kimana negeluni irpayiani le Kimana nepoita orkasolai neishoyo nena plooti*

**Translator:** Kwa mfano, kama kuna ardhi kugawa sehemu ya Kimana tuchaguliwe wazee wa hapa na watu ambao wanahusika wasimamie kugawa ardhi ile.

**Ole Musa:** *ore te wei emirata oo lchambai nikiyiou negeluni ll`payiani le lelo mareita oimua naa ore pee enyamal orpayian neiruhusuni metimira ore pee orpayian ake duo oyieu edaata enye*

**Translator:** Kwa upande wa kuuza ardhi, nataka familia, hata ukoo, ili ile ardhi itakapouzwa ijulikane ni kwa nini iuzwe.

**Ole Musa:** *ore sii enkare keyieu naa enata ake eta entonata eneishori amu ore ninye noolturesh einyalayioki, amu etaa apa enebaya enkare teda abori nemekure taata etumito lelo maasai enkare*

**Translator:** ile chanzo cha Olturesh, kilipotengenezwa na maji yakaenda mbali, sehemu zile nyanda za chini kule Wamaasai siku hizi hawapati maji, ni kukavu.

**Ole Musa:** *neaku eyieu neng`asi aitaraposh lelo tung`ana ootana pee etumi ayaki lelo oolakua*

**Translator:** Maoni yangu ni kwamba wale watu wako pale karibu ambayo hawana maji wapatiwe maji kwanza kabla maji haijapelekwe mbali.

**Ole Musa:** *ore sii ena kop ang kayieu naitayiolo itung`ana ajo ore ena kop eya neyaei ajo ena kop ang memanyai nayeiu naliki intae ajo ekimanya ore ena kop nemeturo naa nkishu nainosita oong`uesi neaku mikiturr kake kiramatishore kigira ake ninye sii yiook ailisha kenya tiai oitoi*

**Translator:** Watu wanasema kwamba nchi ya maasai ni tupu; sio tupu, tuko. Kwa sababu sisi ni watu wa kufuga na vile vili tunakaa na wale wanyama wa pori. Kwa hivyo, tuko na wanyama hapa, hakuna ardhi tupu.

**Ole Musa:** *ore enaa eniking`orita nena ngu`esi nikiyieu sii neing`ori ltung`ana tenerr ing`uesi amuore enaa iniking`orita nena ng`uesi nikiyieu sininche neing`ori il`tung`ana amu kore kuna ropiyiani nagirai alaaki yiook naa torrok amu enelaki nkalifuni tomoniuni tolting`ani naa ninje enyeita il`mong`i lang*

**Translator:** Jinsi tunavyolinda hao wanyama tunawapanda hata wanyama wa pori, ni ajabu kwamba kama mtu akinawa na mnyama, analipwa Sh. 30,000/- kwa ..... (inaudible) Nafikiri hiyo ndiyo sheria ya sasa. Kwa hivyo nimeshangaa.

**Interjection:** Anapendekeza nini?

**Ole Musa:** Yeye anasema mtu akiuwa na mnyama, kiwango cha chini kabisa iwe ni shilingi milioni moja (Shs 1 million)

**Ole Musa:** *ore ene wei oo larikok ayeiu nanu negeluni olarikoni anaa enenyorr il`tung`ana leina area*

**Translator:** Upande wa kiongozi, kiongozi anapochaguliwa achaguliwe na watu wa pale jinsi wapendavyo.

**Ole Musa:** *amu eidim ataa etaoltung`ani enkisuma kake etaa likae ota enkisuma dorrop alang ina naa ninye olarriyia alang oliae*

**Translator:** Inge, kuna mtu ambaye anasoma hali ya juu, na mwingine kisomo duni, lakini kwa upande wa uongozi, huyo ya kisomo duni pengine ana uongozi bora zaidi.

**Ole Musa:** *nayeiu ore laiguanak neoshokini ake siniche kura ashe oleng*

**Translator:** Napendekeza watenda kazi yaani Ma-chief wachaguliwe kwa kura.

**John Nina:** Kwa majina naitwa John Nina. Ningependa kutoa pendekazo langu na yakwanza ni kwamba serikali ione kwamba watoto wote ambao wamefika umri wa kuenda shule walazimishe waende shule na serikali watoe vifaa ambayo walimu wanaweza kufundishia na si cost-sharing. Ningependekeza ile scheme ya ile ya zamani ya Kenya School Equipment Scheme iwe revived.

Ya pili ni Communal Land Tenure system, yaani Shamba la Watu Wengi. Ningependekeza ardhi yote igawanywe na iwe wa individual land tenure system ndiyo mtu aweze kupata title deed na aweze ku-develop pahali yake mwenyewe.

Ya tatu ni kwamba wakati shamba zote zinazwa inapaswa iuzishwe watu wote wa familia hasa mke na watoto. Kwa sababu tuna kuta kwamba saa zingine mzee haana jambo busara au kamili ya kuuza hiyo ardhi, anapenda tu kuuza atumie kwa starehe zake mwenyewe na unakuta kwamba pengine ye ye karibu amalizie umri wake na shida inabakia kwa wale wataachwa nyuma.

Ya nne ni kwamba viongozi kama Ma-Chief na Ma-councilors wawe community wanapewa jikumu wa kuchagua hawa watu. Na atleast wawe na minimum education of form four na factors zingine zikiwa considered.

Ya tano ni kwamba, on the government side, kwa upande wa serikali, senior government officials like the Attorney General, Chief Justice, Solicitor General, hawa wakubwa wakubwa wa serikali isiwe ina-apointiwa na Executive au na President. Iwe ina-apointiwa ama inapendekezwa Executive pamoja na Legislature, yaani Mabunge kwa pamoja.

Sita ni kwamba hao wanyama wa pori wamehangisha wananchi kwa muda mrefu. Na tunaona kwamba, kwa maoni yangu kwamba ni watu wanafungiwa, kama hii area ya Kimana ni watu wamefungiwa kwa eneo na iwe the other way round kwamba ni wanyama wafungiwe kwa sababu hatujaona benefit yake kwa muda mrefu iwe ikiingia kwa mashamba au ikuwa mtu na hiyo

mnyama iuliwe at the spot without consulting the KWS.

Ya saba ni kwamba wakati eneo inapewa tuseme district headquarters ama wilaya, vitu zingine ziangaliwe (some words lost as tape ends) na unakuta kwamba district headquarters iko zaidi ya kilometer 400. Kwa hivyo wa-consider umbali, terrain na other hardship areas.

Nane ni kwamba serikali watenge pesa katika Financial Year waweze kusambaza maji kutoka mto, kutoka lakes na boreholes ndiyo hizi areas za ukame watu waweze kulima walisho mifugo yao, wawe self-sustaining badala ya kuitisha misaada nje.

Tisa ni kwamba leisure time tunaona kwamba ustarehe imeharibu watu wengi hasa community hii, kwamba specific time iwe allocated kwa leisure places. Iwe masaa yanapeanwa kufungwa vitu kama bar, and any other leisure places. Tuseme iwe inafunguliwa kuanzia saa kumi na moja na iwe inafungwa saa nne, kusudi watu waweze kuenda kulala na waweze kuamukia kazi.

Kumi ni kwamba electorals, wale watu wamechagua watu tuseme kama Chief au Councilor ama MP, waweze kupewa uwezo wa kuwa-fire in between their terms. Tuseme kama Mbunge hafanyi kazi, kama Councilor hafaynyi kazi, asiongoje miaka mitano iishe. Wananchi wapewe uwezo waweze kuwa-fire in between their terms.

Ya mwisho kabisa tunaona kwamba ardhi ya Wamaasai tulinyang'wa by the local government, na tunge-need compensation. Ille area tunawenza kurudishiwa turudishiwe, na ile area hatuwezi kurudishiwa tuwe compensated kwa sababu tumenyanyazwa na serikali ya ukoloni na vile vile hatujawekwa vizuri mpaka sasa hivi. Asanteni.

**Julius Kisai:** Mimi ni Julius Kisai, mwalimu. Nina maono haya: kwanza ninaanza na sehemu ya president. President wa nchi, anafaa kutawala kwa miaka kumi tu pekee yake hafai kuongeza zaidi ya miaka kumi, katika uongozi wake. Katika serikali hii yetu, tunaomba kama ingwezekana, tuwe na post ya Prime Minister, na Prime Minister awe anatoka katika opposition katika that ruling party. Ministers wanafaa kuteuliwa na Panel of Members of Parliament, kwa sababu atakuwa akiteuwa Ma-ministers kulingana na upendo wake. Kwa hivyo tunaomba kama ingwezekana, hao ma-ministers wawe wanateuliwa katika parliament, ili tuwe na confidence between ministers ambao wanaweza fanya kazi. Vile vile kama minister hawezি kuwa efficient, awe anabadilishwa after three years, kama anaonekana he is not efficient, anatolewa.

Nikija upande wa education, kuwe na free education katika primary education na katika hiyo free education, vile vile kuwe na subjects vifuatavyo: uwe na science, English, mathematics, GHC and CRE na Kiswahili pekee yake. Hizi subjects zingine ambazo sio examinable katika primary education, ziondolewe, ili zipunguzwe mzigo mkubwa kwa watoto. Katika vile vile status ya education, kuwe na seven years primary education, four years secondary education, na two years form V and form VI na University level kama kawaida. Punishment ya wanafunzi katika shule iwe compulsory; ili kuwe na hudumisaji wa discipline

katika nchi yote. Kwa hivyo watoto wawe disciplined, that is caning, na katika caning, boys should be punished on their buttocks na watoto wasichana wapigwe vidole. Katika education, iwe compulsory kwa watoto wote, hasa katika watu hawa ambao wana hama hama kwa mfano, Wamaasai, Samburu, Wapokot na kadhalika, watoto wote wasome. Huwe compulsory education education kwa wasichana na vijana

Katika upande wa land, ninapoingia sehemu ya ardhi, ni lazima ardhi ikatwe kulingana na occupation wa ya wale watu. Kama watu ni Pastoralists, land iwe shared kulingana na Pastoralism, sababu tukisema iwe 20 acres, ama less than that Pastoralism itakuwa reduced to ground level.

Business, the local government ama the Ministry of Local Government should sponsor the local authority so that licensing katika business ndogo ndogo ikomeshwe kabisa kwa sababu hiyo pesa haionekani pahali inaenda.

Members of Parliament, lazima wawe elected katika the constituencies na hasa wawe wametoka kwa ile constituency. Wamezaliwe kule katika ile constituency na wamelelewa kwa hiyo constituency.

A vote of no confidence should be reflected through the Speaker of the parliament kama huyu member of parliament is not effective. Kama ako effective, the constituents, wanapatiwa ruhusa wam-sack any time.

When it comes to imprisonment, kufunga watu jela, ningeomba kama serikali ingekubalia ama Katiba hii – maono yangu. Ningesema mtu asifungwe zaidi ya miaka 20; kama mtu amefungwa sana isidizi miaka 20, ili huyo mtu arudi tena akishapatiwe ile discipline ya kutosha arudi tena awe Mkenya wa kusaidia wengine.

Ningeomba vile vile death sentence itolewe kwa mtu yoyote anachukua mali ya mtu kwa nguvu, na mtu ambaye anauwa mwengine, that is murdering. Kwa hivyo kama mtu amauwa mwengine, hakuna mambo ya kusema imprisonment ama .... He should also be killed.

When it comes to circumcision of girls, hii itakuwa isiwe compulsory. Kwa sababu other tribes wana traditional beliefs zinatafaa kutolewa; kwa hivyo wanapaswa hiyo circumcision ya girls isiwe compulsory.

On marriage, watoto wasiowane when they are below 18 years; iwekwe sheria ya kwamba watoto wanaowana wakisha fika miaka 18 kuenda mbele; ikiteremka chini, wasiruhusiwe kuowana, kwa sababu ni kama watoto wanaowana.

When it comes to salaries, salaries section, ninaona ni kwamba ni mzuri after every two years, tuwe na salary review katika government workers wote wa Kenya. Kwa hivyo every afer two years, tunakuwa na salary review ya increment ili kuwa-boost wawze kufanya kazi effiently. Minority tribes kama Teso, ndogo ndogo ziwe zina-recognised katika leadership ya Kenya.

Kwa sababu kuna tribes ndogo ndogo kama Wateso, tuseme hizi ambazo haijulikani, ziwe katika government offices, wanaonekana ili wanawenza kutetea watu wao katika sehemu wanatoka

**Interjection:** Mwalimu maliza.

**Mr Kisai:** Sawa. Namaliza na Free market. Free market iwe controlled kabisa. Asante.

**Com.Bishop Njoroge:** Tumeenda .....(inaudible) na tumeambiwa ili kuwe na utawala mzuri lazima tuseparate the Executive, Judiciary na Legislature. Halafu umesema, ma-ministers wakiwe wasiteuliwa na Rais, wateuliwe na Bunge and ministers form the Executive. Are you what ..... parliament. Will that work?

**Mr Kisai** Now I was proposing it will better if these ministers could be elected right from .....

**Com. Lethome:** Next.

**Jackson Mkonyoyo:** Mimi napenda kuzungumza Jina langu ni Jackson Mbonyeo mkaaji hapa Kimana. Napenda kuguzia mambo ya elimu. Elimu iwe ni ya mamlaka. Wamaasai wamesoma, wameendelea wamekuwa graduates, wameenda kila mahali lakini kulingana navile iko, hatuna uongozi. Ukiangalia kama primary, utakuta ni labda ni watu wengine ndiyo wanatuongoza, na hao pia wanawenza.

**Interjection:** Pendeleko?

**Mr Mkonyoyo:** Napendekeza kuwa kwa sababu nao wamesoma, wapewe mamlaka.

Pili, ningependa kusema mambo ya masomo ya lazima. Ikiwezekana, Ma-chief, Wazee mamlaka, walazimize watoto wasome.

Tatu, ningependekeza pia kiboko isiondolewe shulenii maana watoto watakosa nidhamu .

Nne, sisi hapa tunapata na bursaries aina mbili, KWS na County Council. Na bursaries kutoka KWS tunaumia, hakuna kitu tunapata, ni kitu kidogo sana tunapata. Na unaangalia watoto wanatoka porini, wanachelewa shulenii kwa sababu ya wanyama. Na hizo bursaries tunapata through KWS. Hivyo KWS waangalie hizo bursaries tuweze kupewa haki yetu maana

**Interjection:** Mapendeleko?

Napendekeza bursary iende juu maana iko chini zaidi, iongezwe.

**Com. Lethome:** Endelea.

**Mkonyonyo:** Nne, ningependa ku kuzungumzia mambo ya Uongozi kama ya utawala. Kwa mfano Chiefs, iwe ni wamuzi ya wananchi watakayo amua ni nani atakae kuongoza. Kusema mambo ya si mbaya, lakini, unawenza kuchagua mtu mwenye amesoma zaidi na asiongoze wale wananchi. Mfano ni kwamba mambo ya titles. Tumekuwa na shida kuhusu mambo ya title. Unawenza nunua shamba hapa 50,000/- na ukienda kutafuta title, unalipishwa zaidi ya ile pesa tena ambayo umenunua naye shamba.

**Interjection:** Pendelezo?

**Mkonyoyo:** Napendekeza kwamba iangaliwe maana title imeenda juu zaidi.

Ya mwisho, napendekeza pia mambo ya Majimbo

**Com. Lethome:** Kirapeshi Lapawu, afuatwe na Joyce Senewa.

**Kirapashi Lepawu:** Nikianza na mambo ya Katiba, langu la kwanza ni kuhusu Amboseli National Park. Hiyo national park ilienda kwa ile sheria ambaye ilikuwa ya zamani. Na tunaomba, kama sheria ya sasa itaturuhusu sisi wenyewe Wamaasai turudishiwe hiyo eneo, tungependelea kwa maana tunasikia uchungu sana kwa maana faida kubwa inatoka hapo, na sisi wenyewe hatupati. Ile tunapata labda ni kama ni 100% tunapata 30%. Na tungetaka kama haiwezi kurudi, iwe 70% ni yetu, 30% iende mahali ingine.

Mambo ya maji. Kusema kweli hiyo maji ilienda na ilienda kama hatukuwa na mwangaza kwa ajili ilienda na sheria ya zamani. Na tungetaka Katiba ya sasa, kama itaturuhusu sisi wenyewe turudishiwe maji yetu, turudishiwe kwa maana ilienda kwa jina la mtu mmoja na kwa sasa hivi, tunasema tuko zaidi ya watu hata kama ni 1,000 tunasema maji yetu irudishiwe kwa maana inaenda kwa faida ya mtu mmoja na zaidi ya watu 1,000 tunaumia hapa.

**Com. Lethiome:** Endelea kwa point ingine.

**Mkonyonyo:** Jambo la tatu ni kuhusu hawa wanyama wa pori. Kusema ukweli sisi tunakaa na wanyama na kuna watu ambaye wanafaidia naye. Tungeomba kwa vile sisi tunakaa na wao heri tufaidike nayo kwa maana unasilika mtu ameuwawa na ndovu leo, na inakaa muda na inakaa siku nne kuja kuangalia huyo mtu kama amekufa. Lakini saa hii tukipiga ndovu mkuki, saa hiyo unaona ndege inatoka hapa mpaka hapa. Tungeomba mtu kama akiwawa na ndovu alipue zaidi ya milioni 1, kwa maana hiyo ndovu ..... (inaudible).

Jambo lingine ningeomba shule iwe ni ya bure. Kama Katiba hii itatengeneza mambo yote, tafadhali tungeomba kwa maana saa hii maisha ile inatusumbua ni ya watoto wetu. Tungeomba shule ikiwa ni ya bure, tutaona mambo kidogo itakuwa ikabadilika..

Inginge ningezea ni hizi lodges tunayo hapa. Hizi lodges ni yetu, iko pahali yetu ya Maasai na tungeomba wale watakayo ajiriwa kwa hizi ma-lodges, majority ya hawa watu ni sisi wamaasai kwa maana ni area yetu.

Jambo lingine ningeomba, titles za mashamba vile zinatokanga kwa jina ya mzee, mimi ningeomba itoke kwa jina ya mama pamoja na mzee.

Inginge ningeomba, ningeomba kweli kulingana na vile maisha sasa tuko, tungeomba kama shamba itauzwa, ningeomba kama Katiba hii ya leo ambaye inatengenezwa hapa, mambo ya shamba ifungwe, isi uuzwe kabisa. Kwa maana sasa mimi kesho nitakufa, na niuze shamba yote, na wale watoto wangu nitakuwa nimewaachia shida. Hiyo ifungwe kabisa. Kama Katiba hii inaenda kufanya kazi.

Jambo lingine ningeomba kwa upande wa Ma-chief, Madiwani, tungeomba tupewe nafasi ya kuchagua kiongozi ambayo tunawapenda na tunajua watatusaidia. Sio mtu alete mwengine na atuambie huyu mtu ndiyo tumechagua awe Chief. Sisi wenyewe tuchague ndiyo aende akasaidie au aende atusaidie ama amalize .....(inaudible)

Jambo la mwisho ningependa kusema ni kuhusu Wabunge. Tungependa ule Mbunge tutakaye mchagua tutampa nafasi ya miaka tano na kama hajafanya ile kitu, tutaweza kumuondoa kabla miaka tano hiyo haijaisha.

Inginge ningeomba, sisi kweli upande huu tunaona ile mapato inatoka mingi sana inatoka huku Maasaini, kama nyanya, kitunguu, tungeomba kama tungepata soko ilivyo kuenda Mombasa ama kuenda mahali ingine, tungepata soko ya hapa karibu, ingekuwa mzuri sana kwa maana itatusaidia.

Jambao lingine la mwisho, sisi, unajua sisi Wamaasai ni watu wanategemea ng'ombe. Kama tunataka shuka, kama tunataka chakula, mpaka tupeleke mzao sokoni ama ng'ombe. Tungependa tupewe soko ambaye, ng'ombe akipita hapa kupeleka sokoni, itakuwa hata na bei ambaye inaweza kutusaidia. Kwa maana saa hii hapa tunauza ng'ombe hata bei haifai, na tungepata ile soko ambaye inaweza kutusaidia ili ngombe yetu ipate bei ya juu kidogo.

Ya mwisho kabisa ningeomba kama hii Katiba ambaye saa hii kwa maana mashamba yetu imekaa kwa muda mrefu ijakata katwa, hatutaki tupate sehemu inasemekana ni ya watu wote, tunataka ikate katwe kila mtu apate shamba lake. Nafikiri hiyo ndiyo njia nzuri inaweza kutuokoa.

La mwisho kabisa ningeomba kweli hizi ma-petrol ambaye tunaenda kutafuta mahali mbali huko tungeomba hizi station zetu .....(inaudible) tungeweza kupewa hapa ndiyo itakuwa ni jambo la muhimu zaidi.

**Com. Lethome:** Asante. (...inaudible)

**Grace Mwihaki:** Kwa majina mimi naitwa Grace Mwihaki na nimekuja hapa kwa mambo mawili au matatu. Kwa hakika tukiwa wamama tumenyanyaswa sana na hapa ningetaka kusimamia saa hizi ni kwa sababu wamama wengi hawana mabwana, na wana watoto na ni maskini. Ni kwa sababu mtu akikosa bwana ni maskini kwa sababu hana mtu wa kumsaidia. Tumesomesha watoto Primary, tunajikaza na wakulima, tunajikaza na makibarua kwa hao wenye pesa, lakini akifika hata hizo pesa ilibaki mtoto wenu ....(inaudible)

**Interjection:** Sasa unapendekeza nini?

**Mama Grace:** Mimi ningependekeza hivi zamani tulikuwa mtoto akienda University hata kama ni wa maskini anasoma.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo masomo ....(inaudible)

**Mama Grace:** Na siku hizi mtoto hasomi.

**Com. Lethome:** Hiyo tumemaliza.

**Mama Grace:** La pili, ningesema hivi, hapa Kimana Loitokotok kilimo yetu ni ya nyanya, na hizi nyanya tunalima kitungu akina msimamo kwa sababu tumewekewa soko huru, na hiyo soko huru inasaidia watu wa nje.

**Interjection:** Jamani sasa nafikiri tumegeuka .....(inaudible). Wazee, mazungumzo baadaye, .....(inaudible) Machine ita-record kelele. Haya endelea mama. Kama unafikiri unataka kuzungumza, toka nje kidogo halafu ukarudi baadaye. Endelea tu.

**Mama Grace:** Na hiyo soko huru inasaidia wale watu wanatoka nje ya Kenya. Kwa sababu pesa hao wanaenda kuongezea kwao ni nyingi waki-change, lakini sisi Wakenya, tunakosa pesa ya kusomesha watoto.

**Com. Lethome:** Pendekezo. Unasema nini kuhusu free market.

**Mama Grace:** Hiyo mapendekezo zangu ni kwamba hiyo soko kama mnageuza Katiba muifunge.

**Com. Lethome:** Endelea.

**Mama Grace:** Tena tungesema tuwe na usaidizi wa wamama zaidi na zaidi. Ni kwa sababu wamama wale hawana nguvu ya kwenda, .....(inaudible) kupata mambo yao ya masomo au nini, tuwe tukipata ule atakuwa .....(inaudible) karibu na sisi.

**Com. Lethome:** Haya endelea.

**Mama Grace:** Sina la mengine.

**Com. Lethome:** Haya asante sana. ....(inaudible) tulisema asubuhi. Ukiija hapa pendekeza, usitueleze tu matatizo,

usieleze tu matatizo, pendekeza, nataka hivi, nataka hivi. Tutaenda haraka kila moja ambao anataka kuzungumza ....(inaudible). Sasa .... Saiyanga Miria. Haya endelea.

**Saiyanga Miria:** *kaji sayianka miria*

**Translator:** Nataka kuzungumza kwa kifupi sana.

**Mzee Miria:** *ore naa maoni ai edukuya ewaki apa embusel neton apa mikira arriyiak*

**Translator:** Sehemu ya Amboseli ..... (inaudible) tulikuwa bado hatujapata mwangaza wa mambo.

**Mzee Miria:** *ore naa tekuna olong`i ee ena taduo naa ena katiba naa enashukoki loopeny haki enye nikiyieu neshukokini yiook*

**Translator:** Katiba hii sasa tunaiunda ipate haki kwa hivyo turudishiwe sehemu hiyo.

**Mzee Miria:** *ore enkae ore ene weji oo laiguanax keyei nemeitokini agelaki yiook alarikoni leitu kinyorra openy*

**Translator:** Upande wa Ma-chief, vile vile tusirudi kuletewa mtu ambao hatukubali sisi, yaani napendekeza wachaguliwe moja kwa moja.

**Mzee Miria:** *amu ore looti tanakata iji ore oltung`ani, enitum shida oltung`ani neas ake anaa enayieu melo duo anaa shida ino*

**Translator:** Waliopo sasa ukimpelekea shida zako yeye anafanya atakavyo

**Mzee Miria:**

**Translator:** Napendekeza kwamba kwa sababu kwetu kuna watu wamesoma soma, mambo yote, karibu yote yangefanywa na watu wa kuoka hapa.

**Mzee Miria:** *ore enkae naa kiyieu neishori yiook haki ang maitoria openy amu kinoto ilkijanani oisumate , tanaa ilmalimuni neisumate tanaa ldakitarini neisumate nikiyieu naa neishori yiook haki ang maitoria openy*

**Translator:** Wamaasai wamekuwa ni watu wa kutegemea sana ng'ombe na wanyama wa pori.

**Mzee Miria:** *ore naa enkae naa ore apa yiook kibulu yiook ilmaasae naa nkishu kitubulunyie oo ng`uesi , ore det ake too rkulie arin oo tulusoitie nelotu serkali aoru yiook ing`uesi neaku naa ninche nagira adupore mekure apa yiook kiata etaa enerr olng`ojine ing`uesi naa nkalifuni tomoniuni enkine elaki ol`tung`ani nikidol ajo mee haki ina*

**Translator:** Wakati mfupi uliopita serikali imekuja ikatawala wanyama wote kuitia KWS, mtu akifa analipwa Shs.30,000/- na tunaona haifai. Nasema hivi kwa sababu wanyama tumeishi nao. Na ile faida kubwa inatokana ni wale

wanyama iwe ni yetu, kwa sababu ni sisi tunawalinda.

**Mzee Miria:** *naa enemejing`u ina,*

**Translator:** Kama hio haiwezekani

**Mzee Miria:** *neikarra serkali pee meitoki anyikaki yiook*

**Translator:** Serikali iweke .....(inaudible) wanyama wake wanyama wasitukaribie.

**Mzee Miria:** *neina sii enkisuma olmalimuni anaa enkisuma oo nkera*

**Translator:** Kwa masomo ya watoto.

**Mzee Miria:** *oore ilmalimuni naa ilapaitin okuni eisumisha nkera neigoma nejo keyieu neponi olmushara*

**Translator:** Walimu wanakaa kaa kidogo halafu wanaanza kutengeneza mambo ya kugoma ili waongezewe mshahara.

**Mzee Miria:** *ore eponi olmushara neponita ninche fees oo nkera*

**Translator:** Halafu wao wanakuongezea mshahara wao wanaongezea karo ya shule.

**Mzee Miria:** *nikidol ajo ore sininye ina kiyieu enemeidim sii naji ena katiba atabala nkera meisumata pesho neaku, naji enkiti toki kilak*

**Translator:** Kama hii Katiba haitapeana masomo ya bure, basi ipunguze karo kabisa kwa kiwango cha chini iwezekanavyo.

**Mzee Miria:** *neina enkare e pipeline*

**Translator:** Nataka maji ya Bomba kuu.

**Mzee Miria:** *ewaki apa ina are too nkolong`i natana kake mikiyiolo sii yiook anaa kapa eishoyioki ina are anaa keidim atushukoki yioook olapa pipe musana*

**Translator:** Na haya maji ilichukuliwa sijui kwa mtindo gani lakini anaomba hivi kwamba, kama yale maji yangerudishwa ile bomba ya zamani .....(inaudible) kama ingewezekana hiyo bomba ingeweza kusaidia watu wengi.

**Mzee Miria:** *ore apa olapa keju oim enkare mekure taata eim*

**Translator:** Ile kitu yote ilikuwa inapita maji wakati huo siku hizi hakuna maji.

**Mzee Miria:** *nejo serkali ore orkeju naa ole serkali ore enkare naa ne serkali*

**Translator:** Serikali inasema rasilimali yote mto pamoja na maji ni ya serikali.

**Mzee Miria:** *kining`ito ajo likae tun`gani ogira adupore etung`ayie apa loopeny*

**Translator:** Anasikia kwamba maji aliondokea wenyewe anapatia faida watu wengine mbali.

**Com. Lethome:** Pendekeza.

**Mzee Miria:** *kiyieu ore ina are ore pee elo kilomita emiet nepiki enkare nikiok pesho*

**Translator:** Bomba ile inapokamilika n..... basi tuwekewe t..... ama ijaziwe na maji.

**Mzee Miria:** *ore taa nanu naa ine aitabaiki*

**Translator:** Mimi nafika hapo.

**Com. Lethome:** Asante sana. Joyce Senewa.

**Joseph Senewa:** Kwa majina yangu ni Joyce Senewa na mimi ni member ya CCC na ya kwanza ningeongea kuhusu muongozo wa Katiba, Preamble. Ningependeka Katiba mpya iweze kuwa na utangulizi ambao kuna shirikisha kila unashirikisha kila kabila la Kenya na hata iweze kushilikisha maono ya wa Kenya na iandikwe kwa kabila tofauti ili kila mtu aweze kuelewa Katiba inasemaje na inamlinda na njia gani.

Ya pili ningeongea kuhusu vyama vya siasa; hizi ziweze kupunguzwa viwe viwili tu katika Kenya ili tuweze kuzuia watu kuchanganyikiwa na kukosa muelekeo. Halafu ya pili katika vyama vya siasa, kila chama ambacho ni cha siasa iweze kujitafutia fedha zake za matumishi.

Katika Bunge ningependekeza ya kwamba, anaye wania Urais awe ni mtu ambaye amesoma, ako na Diploma na pia amefanya kazi kwa muda wa miaka tano. Na pia awe na sifa nzuri, awe ni mtu ana boma na pia awe na miaka 40 mwanzo na mwisho iwe ni miaka 70. Pia katika Bunge ningependekeza tusiweko na kuteuliwa kwa Ma-councilor au MP. Halafu katika Bunge ningesema iwekwe sheria Katiba inayo sema ya kwamba 1/3 theluji tatu ya Wabunge iwe ni wamama.

Muundo wa utaratibu wa uchaguzi; ningependa kuwe na viti ambavyo vimewekwa kando kwa sababu ya vikundi kama wamama na wasiojiweza.

Halafu pia mpaka ya constituency iweze kurudiwa kwa sababu tuna constituencies zingine kubwa kama hii yetu ya Kajiado, ambaye ingefaa kuwa na district mbili.

Halafu ningependekeza pia kwa sababu wanao ishi Kajiado ni watu wa kuhama hama, kuwe pia wakati wa kura kuna Mobile polling stations, yaani pahali ya kupigia kura inayo zunguka, kufuata wafugaji mahali walipo.

Haki za binadamu – Basic Rights; ningependekeza kwamba, Katiba iweze kulinda haki za watu. Katika elimu tuwe na masomo ya bure kwanzia nursery hadi standard eight. Na pia fees ya secondary school iweze kupunguzwa ili kuwezesha maskini waweze kupata elimu. Katika hali ya health, yaani afya, kuwe na hospitali za bure, yaani matibabu iwe ni bure. Kuwe na mobile hospitals ambao zinazunguka kufuata watu maana ni wafugaji. Halafu maana Rais alitangaza ya kwamba Ukimwi umekuwa ni janga la taifa, kuweze kuwa na Machine za Western Blot katika kila district hospital ili kuweza kufamisha watu kwa haraka kwamba ni vini.

Katika security, ningependekeza ya kwamba, polisi anaposhika mtu, huyo mtu asiadhibiwe mpaka aweze kubalika kwamba ako na makosa. Pia polisi akishika mtu, huyu mtu asifunguwe kwa ofisi ya cell, hapa kwa ofisi ya Chief, zaidi ya siku tatu, kabla haijapelekwa kwa Judge. Na pia hata akipelekwa kama ni Loitokitok kwa cell, anafungiwa siku mbili na ya tatu iwe anapelekwa mahakamani asikae zaidi ya siku tatu.

Mambo ya soko huru; ningependekeza ya kwamba kulingana na wakulima wanao lima vitu za horticultural kama nyanya na vitunguu, soko huru isiwekwe maana inaumiza sana na inachokeza watu hata faida hawawezi kujimudu kimaisha.

Land Property Rights; ningependekeza ya kwamba, ardhi iweze kumilikiwa na wenyewe na jamii, yaani community.

Ya pili ningependekeza Land Board isiwepo, na kuwe na Board ambayo ni ya wazee wa ma boma, yaani Local Land Board ya community. Halafu uzaji wa shamba usiwepo na usikubalike mpaka wazazi mama na baba wakubaliane pamoja na watoto. Wamama waweze kuriithi mashamba na wasichana ambao hawajaolewa. Pia wazee waweze kugawia wamama mali, ingali wakiwa hai. Halafu pia ningependekeza ya kwamba ile makubaliano kati ya Lenana na Wazungu ya kwamba watakapo ondoka warudishie Wamaasai shamba yao, ilikuwa 1911, serikali iweze kukubali ya kwamba hiyo treaty ilikuweko, na baada ya hao ningependekeza Wamaasai waweze kuunda Commission ambayo itachunguza jinsi watakavyo regesewa au wawe compensated katika hiyo miaka ambayo watu wengine wametumia hiyo haki yao.

Ningeomba kwama maana kuna Makampuni ya Kahawa, Ma-factory ya Kahawa na Majani, KMC iweze kurejezwa na ufunguliwe matawi katika kila pahali kuna wafugaji ili wafugaji waweze kupata mahali pa kuuza wanyama.

Ningependekeza pia katika Culture and ethnicity – yaani mila, community iweze ku.... (inaudible) mila ambazo zinawasaidia. Na kuwe na Katiba ambao inaweza ku-protect mila na rasilimali. Ni hayo tu.

**Com. Lethome:** Asanti sana Joyce. Salisipa Lasanga, afuatue na Martine Kirau ..... (inaudible)

**Salisipa Lasanga:** *ore taa ena dukuya naa airoroki intae sarimpa parsanka*

**Translator:** Jina langu ni Salisipa Lasanga.

**Mr Lasanga:** *ore naa enai naa enkirorokino airoroki larikok oetuo tonalakua oo olooetuo tenetana*

**Translator:** Viongozi waliotoka mbali na walioko hapa.

**Mr Lasanga:** *ore naa enkiroroto naa ena duo nayawua yiook ene*

**Translator:** Anaelekea kuwazungumzia walio hapa.

**Mr Lasanga:** *naa or sinanu enasuj naa ketii ninye likae turrurr lasuj kake alimu sinanu inkutiti*

**Translator:** Ijapokuwa wengi wamesema mimi nina machache

**Mr Lasanga:** *naa kore ene dukuya naa kinyor ena siai naleng oo kuna kuapi ang najeito majjeito am kidolita naa osina sapuk anaa pee elo*

**Translator:** Mimi napenda sana kuzumgumzia mambo ya ardhi watu wengi walio ....(inaudible)

**Mr Lasanga:** *amu ore ena siai taata nayawua enyamali sapuk naa enasiai naji ejii enelo taata oltungani inkopisini , neelo aiger entoki neitu sii ening`okino ena raia pooki nikidol ajo ninye nagira ayau enyamali sapuk*

**Translator:** Naona kuna shida mtu akiuza ardhi ama akifanya mambo ya ardhi akenda ma-ofisini ana ..... huku na kule.

**Mr Lasanga:** *amu enegeluni olarikoni ogeluni raia, neishori sinenche raia egolon anaa taata tenasiai oo kuna opisini naa lio ajo ena siai oo ilchambai nikinyorr enening`okino intoiwuo pooki amu inakata kitum pooki ena kop, amu ore taata ene weiji e landboard tenepiki kenya lpayiani meeta mikintoki ajo kipou anaa nkopisini oldioo, nikidol ajo ore ina toki neisho yiook egolon sapuk meshomo ena kop ang dukuya*

**Translator:** Napendekeza kwamba wale wamehuskika na mambo ya kusimamia ardhi wawe wanateuliwa ama kuchagaliwa na wananchi wa pale ama ile jamii ya pale. Kama tungepata wazee wa kutoka jamii yetu, na watu wengine ambao tunashirikiana vizuri, hatuta kuwa na haja ya kwenda kusumbiliwa na kwa mambo ya ardhi.

**Mr Lasanga:** *ore sii ena sia natio ajo enoo ng`uesi , tenebo olkeek ore duo yiook anaa kiramatisho oshi lmaasai nikijo inkunaang amu enkopang etii*

**Translator:** Nageukia mambo ya wanyama na pori. Sisi uwa tunafikiria kwamba wanyama na mambo ya pori ni mali yetu.

**Mr Lasanga:** *nikidol ajo tenerr oltung`ani eng`ues, ore sii nai pee epuo olkiyioi nemeikoni ilo tung`ani anaa ina apa ajo anaa ina apa naikoni nena ng`uesi*

**Translator:** Lakini ni ya ajabu kwamba kama mtu akiuwa kwa mfano na mnyama na upeleke kilio chako haungaliwi hata kidogo kwa hivyo ina .....(inaudible).

**Mr Lasanga:** *ore sii pee kiyiou ena siaai natio ajo enoolchambai nneitashayieki, etejo apa ebaiki apa nejo l`tung`ani otaa lapa shambai musan amirr amau atum scheme*

**Translator:** Kwa sababu ya sisi kusema mashamba ..... (inaudible) ni kwamba, watu wengine waliuza mashamba wakitarajia kwamba wataenda kupatiwa sehemu katika mashamba makuu tunaita Group Ranches.

**Com. Lethome:** Pendekezo

**Mr Lasanga:** *ore naa ena taata naaene mwisho*

**Translator:** Hii iwe ya mwisho.

**Mr Lasanga:** *eta oshi entoki najo ilmaasai entast olpayian etai edung`oret*

**Translator:** zee na mke wake wanasema kwamba hakuna kitu cha kuriidhi

**Mr Lasanga:** *naa enemirr naa taata ena niaku olmanambai nintoki ayau enyamali te kurum*

**Translator:** Naona kwamba hii ardhi ikienda watu watakuja ku.....(inaudible) na kukaa bila kazi.

**Mr Lasanga:** *neaku naa taata kijo tenemutu eaku ena katiba ang anaa ena neaku enapa najo l`maasai epik emongoi inkishu boo neshuku esipata*

**Translator:** Kama Katiba itakubali mhaki analete ng'ombe kwa boma halafu muongo unaondoa ng'ombe kwa boma.

**Mr Lasanga:** *ore sii larikok lang etii naji ltung`ana lojo kiyiu ltung`ani oisume nkilasini sapukin tenewei e council*

**Translator:** Nkiongea upande wa Viongozi kama Madiwani,

**Mr Lasanga:** *tenebo oo laiguanax pee kioshoki kura*

**Translator:** Vile vile Ma-chief napendekeza kwamba wapigiwe kura.

**Mr Lasanga:** *nikijo yiiok enyorrata oo l`tauja, nalo ajo neija amu ore toi sii oloisume nelo aaku olowaru*

*neaku enkalamu earie iltung`anak nikidol ajo merikito yiook ilo*

**Translator:** Naunga mkono mama ambaye alisema amesoma akichaguliwa anaweza mtu wa kumaliza wengine.

**Mr Lasanga:** *kake tenetoni ore apake ilmaasai anaa tebulunoto kining`ito sii yiook, tenetoni apake neji mategelu ele tung`ani, nenyor enkai nenyor enkop*

**Translator:** Lakini kama jamii imependekeza mtu wa kumchagua mtu, yule mtu ataenda kuwaletea makazo.

**Mr Lasanga:** *kake etaa taata tenejokini oltung`ani esipata, neipirri elo nelo opisi netum entoki naihongayie amu elo naa dukuya enkoitoe nemeyiolo irkumok nelo ajo esipata neme enatejoki nelo ninye adung`u enenye*

**Translator:** Lakini hawa wamesema wamesoma hawa ndiyo .....(inaudible)

**Com. Lethome:** Toa pendekeza.

**Mr Lasanga:** *naa ninye naa ajo iji kajo yiook omokiadolisho tenyorrata oo l`tauja*

**Translator:** Sisi ndiyo tumekuwa tukiwachagua

**Mr Lasanga:** *meeta ashuku enashe sapuk enaa enikinchoo pee maitoki aiturraa ildaikani*

**Translator:** Kwa hivyo ninashukuru ..... (inaudible) Nafika hapo. Asante.

**Com. Lethome:** (Inaudible)

**Martine Kirau:** *ore naa enkarna naa martine naa kra assistant chief te nchoto ee mbusel sublocation*

**Translator:** Mimi ni Martine na ni Chief mdogo kutoka upande wa Amboseli.

**Mr Kirau:** alo naa nanu airo ong`uan nijo kuna

**Translator:** Niko na mambo manne tu.

**Mr Kirau:** *ore ene dukuya naa esiai e nkop*

**Translator:** Kwanza ni mambo ya ardhi.

**Mr Kirau:** *ore e siai e nkop nayieu nanu neikoni iji*

**Translator:** Napendekeza mambo ya ardhi uwe ni mtindo huu.

**Mr Kirau:** *ore emirata enkop amu mepal ake il`tung`ana nemookini aiteru ake te committee olpayiani le sub-location nepuoi location nepuoi division*

**Translator:** Mambo ya kuuza ardhi haitaachwa lakini mtindo anapendekeza mtindo iwe namna hii; ianze kwa jamii ikielekea juu.

**Mr Kirau:** *ore ene are*

**Translator:** Ya pili

**Mr Kirau:** *naa esiai entonata oo l`tung`ana too losho lenye*

**Translator:** Ni mambo ya watu kukaa sehemu zao

**Mr Kirau:** *naa pee etoni l`maasai to losho lenye anaa l`maasai openy enkop*

**Translator:** Napendekeza Wamaasai wabaki kama Wamaasai katika sehemu yao. Kama wananchi wa pale.

**Mr Kirau:** *ore ntokitin pooki sidan anaa erikore, oo nena kulio pooki neaku ake nkunenye anaa enenye enkop*

**Translator:** Uongozi aina yoyote uwe ni wa watu wa pale, Wamaasai wenyewe.

**Mr Kirau:** *ore ene uni naa baishara*

**Translator:** Halafu ya tatu ni mambo ya biashara.

**Mr Kirau:** *tenetaa serkali uesto neitobiraki l`tung`ana osokoni loo nkishu tena wilaya ndogo oloitokitok*

**Translator:** Hii serikali iiao inaulizwa kama inauwezo iweze kutengenezea wafugaji masoko.

**Mr Kirau:** *ore ene mwisho naa*

**Translator:** Halafu ya mwisho kabisa,

**Mr Kirau:** *esiai enkare*

**Translator:** Ni taabu ya maji.

**Mr Kirau:** *ore taa ena najiake neai noolturesh, neitunguari iltu`ng`ana ekesipa,*

**Translator:** Hii mambo yanasmekana ni mambo ya .....(inaudible) imechukuliwa huo ni ukweli mtupu.

**Mr Kirau:** *amu enemutu apa etuduoki enaa wetin neenyikinyika pee etum ilopeny enkare neishakinore*

**Translator:** Kama ingepatikana maji karibu na wale watu hio ingekuwa inafaa.

**Mr Kirau:** *ore ene mwisho naa enasiai narita ng`uesi l`tung`ana*

**Translator:** Na hii mambo ya wanyama kuuwa watu,

**Mr Kirau:** naa sidai naaji amu ore duat ainei naa sidai pee etumi alak il`tung`ana emillion

**Translator:** Mapendekezo langu ni kwamba mtu asilipue chini ya Sh. 1 million za Kenya.

**Mr Kirau:** ore naa en mwisho kabisa naa esiai e nkisuma,

**Translator:** Mwisho kabisa ni mambo ya masomo.

**Mr Kirau:** or enkisuma neiyieu nemut serkali alaaki unkera enkisuma iateru te darasa e dukaya mbaka ene isiet

**Translator:** Watu wanapendekeza shule za msingi, serikali ichukue jukumu hilo wale wananchi wasilipe chochote.

**Mr Kirau:** ore esiai e rikore

**Translator:** Mambo ya uongozi.

**Mr Kirau:** naa enejo ol`tung`ana naa mbaka ake ol`tung`ani ake oisume ashu mbaka naa enaje naa eitegemea naa ol`tung`ani onyor il`tuung`ana

**Translator:** Mtu alisema kwamba wale waliosoma ndiyo wapate uongozi lakini mimi kwa upande wangu naona kwamba Kiongozi ategemee anacho pendwa na watu wake.

**Mr Kirau:** amaa enemikinyor il`tung`ana ijing`u naa?

**Translator:** Kama umesoma hata kama uko na degree ngapi na watu hawakupendi, utaingia je uongozi?

**Mr Kirau:** naa ore naa enkoitoi naa ina nanu alotie naaolt`ung`ani kirotet tooltung`ana ninye eishokinore erikore

**Translator:** Yule ki-penzi wa ujamii ndiyo wapewe uongozi

**Mr Kirau:** eisume woitu eisuma

**Translator:** Na akiwa amesoma wala hajasoma

**Mr Kirau:** enaikash teneponu too nena kuapi natii neing`uueki loopeny metotonie

**Com. Lethome.** Ngoja swali moja mzee. Wamaasai wakae sehemu yao, na watu wengine wakae kwao. Sasa si hii italeta ukabila kati ya Maasai wale wa ..... (Inaudible)

**Mr Kirau:** kiyieu enkop ang

**Translator:** Afadhalu wafukuze.....(inaudible) Hiyo ni maoni yangu.

**Meibuko Ntawasa:** Mimi naitwa Ntawasa Meibuko na maoni yangu ya kwanza ni kuhusu mambo ya elimu.

**Interjection:** Ebu kimia kidogo. Endelea.

**Mr Ntawasa:** Langu la kwanza ni kuhusu mambo ya elimu, hasa katika masomo ya shule za msingi. Shule za msingi ziwe zinasomesha watoto bure, kuanzia madarasa ya chini, nursery mpaka darasa la nane, iwe ni masomo ya bure. Na pia hapo hapo kuwe na ulazime ya kila mtu asomeshe mtoto. Kwa hivyo serikali itumie nguvu kwa wale ambao hawataki kuweka watoto wao shuleni ili watoto wapate elimu. Na pia katika (*some words lost as tape ends*) apate kupata elimu yake mara ni wengi kwa kweli wanaweza kusomesha hata kwa masomo hasa haya ya msingi lakini kufika secondary unakuta mambo inakuwa ni magumu. Kwa hivyo tunahitaji msaada hapo serikali ituangalie.

Pia kuhusu mambo ya ardhi hasa upande wa hii Committee ya Land Control Board. Hiyo tunataka iwe inatoka katika jamii ya mahali pale hasa hapa kwetu sisi Wamaasai tunahitaji iwe ni sisi ndiyo tunakaa tunachagua wale ambao tunawapenda wapate kuenda kutusaidia katika mambo hayo. Na pia iwe na Kamati mara mbili. Kuwe katika Kata, kata ndogo, na pia katika Kat. Kuwe na hizo kamati mbili ambazo hawa wa kata ndogo kwanza wazungumze jambo hilo, ndiyo sasa ipate kupelekwa mbele ijulikane jambo hilo ni sawa, basi ipate kutekelezwa. Lakini pia kuwe na makubaliano ya jamii kwa jumla, yaani familia.

Kuhusu mambo ya wanyama, tulikuwa na sehemu hiyo ya Amboseli ambaye imeweza kuchukuliwa zamani na labda haikuenda kwa maoni ya watu wengi. Labda ni watu wachache walikaa na kukubaliana iende hivyo. Lakini sasa kwa sababu ya hao, mambo haya ambayo Katiba ambaye tunabadlisha, tunataka hiyo Amboseli irudi kwetu sisi wenyeji, hasa iwe chini yetu sisi Wamaasai, na pia hapo, hapo, na pia hapo hapo. Wale ambao wanaolinda wale wanyama iwe ni watu wa mahali pale. Maana sasa hivi unawenza kuangalia kwamba hawa wanyama wale ambayo wameajiriwa pale wengi si watu ambaye wametoka sehemu hii; kuwe ni usawa ama iwe asili mia kubwa ni ya watu ambaye wametoka katika jamii ya mahali pale wanyama waporini wanapatikana.

Inginge katika mambo ya utawala, ni mimi kwa maoni yangu naona kwamba serikali ya Majimbo ni nzuri; maana sasa hawa wanyama waporini unakuta wanatuingizia shida nyingi sana. Lakini hizo pesa ambaye inaweza kuja kutufikia sisi, unakuta unakuta ni pesa kidogo sana ambao haiwezi kusaidia. Lakini tukipata serikali hii ya Majimbo, utakuta zile fedha zote zinaweza kurudi na wenyeji wa mahali pale watakuja wakae na wajadiliane hiyo pesa itatumika kwa namna gani, maana watu wengi wanauwawa na wanyama, unakuta mtu hata mwingine hazugulikiwi lakini mnyama saa hii ikipata ajali yoyote, unakuta hata mpaka mengi zinatoa mahali pale. Lakini kama ni mwanadamu hakuna hatua yoyote inachukuliwa. Kwa hivyo tungependa kwamba tupate serikali hii ya Majimbo ili tupate sisi wenyeje kujitawala na kujiangalia katika mambo haya.

Katika mambo ya uajiri, ningependekeza kwamba kuwe na usawa wa makabila yote, hata kama ni Jeshi la Kenya. Labda ni khabila moja ndiyo imechukua jukumu ya kuweza kuajiri watu wengi, kwa hivyo hata sisi tunahitaji ya kwamba tuwe na watu

ambao wata weza kuenda kuajiriwa katika mahali pale kwa maana watu wengi wamesoma na unakuta sasa wanarudi wanaanza kulima na pia hiyo kilimo hata haitusaidii saa hii kulingana na hiyo soko huru; kwa hivyo tunahitaji kama ni hiyo soko huru, serikali iangalie ili kama kuna hiyo soko huru maana hao ndiyo wanakuja na wanaletea mkulima hasara, analima na anakosa hiyo mapato yake. Serikali iangalie ili ijulikane ni kwa njia gani mkulima anaweza kufaidika. Kwa hivyo yangu ni hayo.

**Com. Lethome:** Asante sana. William. William Meikoki. Afuate na Stephen Karanja.

**William Meikoki:** Basi kwa majina yangu ni William Meikoki. Mimi nina jambo moja, mapendekezo yangu, ya kwanza ni kuhusu ardhi. Ardhi kwa hakika sisi Wamaasai tumenyanyaswa kwa upande wa ardhi. Kwa sababu ukiangalia kama vile Amboseli haikwenda kwa njia ambaye inastahili. ....(inaudible) imenyanyaswa. Babu zetu ndiyo walinyanyaswa wakaambiwa kwamba hapa tutakaa pamoja. Ningependa Amboseli irudi kwa mkono ya wenyeji.

La pili, pia kuna sehemu kama Magadi, ambaye ni Kampuni kubwa inalete pesa nyingi kwa nchi hii. Pia hapo ingerudishwa kwa mkono ya wenyeji.

Tatu ni serikali, admnistration; kwa upande wa serikali pia tungependa tuwe na wenyeji. Sisi pia Wamaasai tumepata vijana wamesoma hata graduates we have now, ambao wanaweza kumiliki hizo makazi.

**Interjection:** (Inaudible)

**Mr Meikoki:** Locals kuanzia province.

**Com. Lethome:** From PC, awe ni Maasai?

**Mr Meikoki:** Awe ni Maasai

**Com. Lethome:** Rift Valley iko na Wakalenjin ndani yake, Maasai, Pokot, Turkana.

**Mr Meikoki:** Okay, wacha iwe district level.

**Com. Lethome:** Okay, kuanzia DC mpaka Chief.

**Mr Meikoki:** Mpaka Chief. Ya nne, ni masomo. Masomo iwe sana kwa msichana na kijana. Kwa kusema hii, wasichana wa Kimaasai wamenyanyswa kimasomo. Hao pia ni watu wa kutoka jamii, kwa hivyo nao ni watu wanafaa wapatiwe masomo, vile vile vijana wanapatiwa. Ili sisi wakati mwingine tukija mahali kama hapa tuwe na Commissioners wasichana, tuwe na secretary ambao anaweza kutuwakilishia mahali kama hapa.

Ya tano, ni masilahi ya wafugaji. Kwa hakika wafugaji, sisi tumenyanyaswa kabisa; kwa vile tunasikia budget ya kahawa, kuna mambo mengine mapangilio kama majani chai, na sisi pia nadhani katika dunia mzima hakuna mtu akulangi nyama. Kila moja anapenda nyama, isipokuwa wengine. Basi kwa hivyo, hawa Maasai wapewe uhuru, tufunguliwe viwanda kama vile KMC, na mengine mingi na soko tuwekewe hapa. Mambo ya cess tisiwe nayo, kwa sababu mali ni yetu, ardhi ni yetu, kwa hivyo hii mambo ya cess kwa ng'ombe mimi sioni haja.

Basi langu la mwisho, ni hii mambo ya serikali, mseto, serikali ya mseto, nimanisha Majimbosm. Hii serikali pia tuwe nayo kwa sababu mimi naonelea ni vizuri.

**Interjection:** Pendekeza ..... (inaudible) coalition government unajua kuna mseto.

**Mr Meikoki:** I mean coalition.

**Com. Lethome:** Coalition.

**Mr Meikoki:** Basi ninapenda hii coalition, tuwe na vyama kama mbili, na mtu kama vice president atoke kwa upande wa Upinzani ama Prime Minister. Na katika Bunge tuwe pia na representatives kama vile vijana, mtu wa kutoka kwa vijana na wamama pia wakilishwe.

**Com. Lethome:** Kijana ni nani, hukusema umri wa kijana.

**Mr Meikoki:** Kijana namaanisha kijana tukiwa pamoja wasichana na

**Com. Lethome:** Age.

**Meikoki:** Okay, okay, kuanzia 18 kwenda mbele, mpaka 30.

**Com. Lethome:** Mpaka 30. Chini 18 na 30 ni juu. Kwa hivyo ..... (inaudible). Asante sana. Stephen Karanja, afuatiwe na Mainga Raymond George.

**Stephen Karanja:** Majina yangu ni Stephen Karanja na mimi ni mkulima. Kulingana na hii mambo ya Katiba, ningenzia na Executive. Ningependekeza uchaguzi ifanyike kwa section mbili. Ikuwe section mbili. Section ya kwanza tuwe na Madiwani na Wabunge ifanywe siku hiyo moja. Na siku ya pili, au siku ambaye itakuwa inafuatia, tuwe na uchaguzi wa Rais. Lakini zote siwe zinaenda pamoja. Napendekeza pia tuwe na uchaguzi wa Rais, hii nime-cover. Ingine ni parastatal; viongozi wa parastatals wawe wakichaguliwa na rahia, lakini sio wawe wakichaguliwa na kiongozi wa nchi.

Ile ingine ni mambo ya County Council. Iko na mambo mengi inapatia nchi hii pesa, na ningependa County Council ipatiwe mamlaka ya kuchungua hizo pesa, wawe waki-improve barabara, ma-hospitali na mambo mengine. Kwa hivyo kama ni hii mambo ya maji, iwe ikiuzwa, na County Council inachukua hiyo pesa na inafanya wananchi kazi.

Ingine ni pahali ya worship. Freedom of worship. Serikali ilitoa freedom of worship na haikupendekeza ni worship ya aina gani. Ningependekeza worship iwe inapendekezwa ni ile ya kuabudu Mungu, lakini sio ya kuabudu shetani. Hiyo ni moja ambaye tumeone imeenda vibaya.

Kwa upande wa education, tungependekeza ile education ya zamani ile ilikuwa ya Carey Francis irudiwe. Vitabu vile ziliikuwa

zinatumika na kuanzia standard one hadi form six iwe unafutiliwa, ili hii duplication ya kuwa na syllabus mwaka huu na mwaka ile ingine iwe imeondolewa. Na system itakuwa mzuri.

Ile ingine ni mambo ya Provincial Administration; Chief wawe wakichaguliwa na rahi na wawe wakipigwa transfer hapa na pale kama Civil servant mwingine yejote. Wasiwe tu ni hapo hapo tu, ambaye wanafanya kazi.

**Interjection:** Wanachaguliwa kwenye location?

**Bw Karanja:** Location

**Com. Lethome:** Halafu unasema anaenda kupigwa transfer? Sasa kwa mfano ..... Watu wamechagua, halafu yule mtu wamechagua anakuwa transferred anapelekwa location ingine?

**Bw Karanja:** Akikaa hapa anaweza kaa kwa muda halafu anapelekwa kwa location ingine.

**Com. Lethome:** Watamchague .....(inaudible)

**Bw Karanja:** Watamchagua hao ..... watachukua wao.

**Com Lethome:** Kwa hivyo wanaweza kuwa transferred .....(Inaudible)

**Bw. Karanja:** DC wawe wawe wametoka katika mkoa huo ambaye wako na mambo itakuwa mzuri. Inge ni mambo ya National water corporation ; wananchi wa area pahali maji imetoka wapatiwe first priority ya maji kwanza kabla haijaenda pahali ingine. Jambo ile ingine ni mambo ya agriculture. Agriculture ningependekeza ile mara ya zamani irudishwe, ile mara wakulima wawe wanapatiwa mikopo na kama ina fail wanapatiwa tu mpaka wafafulu. Kwa hivyo ningependekeza ile GMR ya zamani irudishwe. Nafikiri sina mengi na hayo tu.

**Com: Lethome:** Asante. Mzee alijaribu kua..... (inaudible) akasema nafasi, kwa sababu ya mambo ya katiba akakuja mpaka hapa. Mheshimiwa sasa nitakupa nafasi.

**Mhe. Philip Ole Singaru:** Kwa majina Bw. Commissioner ni Philip Ole Singatu. Yangu Majimboism. Mimi siungu Majimbo mkono kamue; kwa sababu nchi nyingi ya Africa imevunjwa na ukabila. Na ikiwa nchi inavunjwa na ukabila, na jee taifa moja, ikigawanyika gawanyika kikundi, kwa sababu ya tamaa ya uongozi. Tunataka umoja wa taifa ambayo haina magawanyiko ndani. Na hiyo ndiyo inaweza kuangalia masilahi na kuleta umoja kamili katika taifa. Maana Majimbo, naona kabila ni cancer katika Africa, ime.....(inaudible). Kwa hivyo, tusijaribu jambo hilo kwa sababu itatugawanya into pieces, na hatuta kuwa na imani kamwe.

**Interjection:** Next point.

